na hali halisi yenye mvuto na kampeni za uhamasishaji kwenye vyombo vya habari. Kampeni hizo zina mlengo wa kubadili tabia za watu wanaotumia barabara. Aidha, Shirika, hufanya kazi moja kwa moja na tasnia ya wanahabari ili kujua ukubwa wa tatizo, majeruhi , vifo na madhara kwa afya ya jamii.

- **Taarifa fupi kutoka mataifa mbalimbali**

Urusi: Utekelezaji wa sheria kali na kampeni za vyombo vya habari imesaidia sana kuongeza viwango vya uvaaji wa mikanda kati ya mwaka 2010 na 2013, mjini Lipetsk Oblast kiwango kimeongezeka kutoka asilimia 50 hadi karibu asilimia 80.Katika mji wa Ivanovo Oblast kiwango kimeongezeka kutoka asilimia 50 hadi asilimia 90. Kadhalika, matumizi ya vizuizi vya watoto yameongezeka kwa mara nne zaidi katika mji wa Oblast kutoka asilimia 20 hadi asilimia 80 .

Vietnam: Serikali ya Vietnam ikishirikiana na WHO imeendeleza kampeni ya kuboresha sheria na kanuni za usalama barabarani toka 2007; Nchi hiyo imeendelea kuhimiza uvaaji wa kofia ngumu miongoni mwa waendesha pikipiki. Sheria pia inawajibisha wazazi kuhakikisha kwamba watoto wao wanavaa kofia ngumu wanapokuwa abiria au kuendesha pikipiki; Aidha, kumekuwa na ongezeko la faini; kuweka sheria kali kuhakikisha kwamba madereva na abiria wa pikipiki wanavaa kofia ngumu zenye viwango vinavyotakiwa kimataifa. Uvaaji wa kofia ngumu uliongezeka kutoka asilimia 40.1 mwaka 2007 hadi zaidi ya asilimia 90 mwaka 2008 na umeendelea kubaki kwenye asilimia 90 tangu kuanzishwa kwa sheria ya kofia ngumu za pikipiki mwaka 2007.



Kampeni za Vyombo vya Habari: Kampeni za kijamii zilizofanyiwa utafiti na ushahidi wa kutosha zina nafasi au ushawishi mkubwa wa kubadilisha tabia na mitazamo ya watu kuhusu suala la usalama barabarani. Tafiti zimeonyesha kwamba matangazo ambayo yana mvuto kwa jamii ni yale yenye kuonyesha hali halisi na ukweli ulivyo barabarani kwani yanakumbukwa vizuri na walengwa. Shirika ,limejitolea kutoa msaada kwenye maeneo ya kampeni ya kubadili tabia za watu katika nchi kama Brazil, Cambodia, Kenya na Mexico zimehama kutoka "*kampeni za kawaida*" kwenda katika matangazo makali yanayolenga *kubadili mitazamo na kufuata sheria.*

Maelezo ya picha: *Shirika la Afya Duniani (WHO) limetengeneza maktaba ya mtandaoni yenye matangazo ya radio na Televisheni kuhusu usalama yaliyopo sasa kutoka pande zote za dunia ili kuhimiza na kuwagusa wanaoanzisha kampeni mpya kwenye nchi zao*

Kupata Wataalamu: Shirika linaratibu mpango wa usalama barabarani kupitia Umoja wa Mataifa na kusaidia vyombo vya habari kupata habari za usalama barabarani na wataalamu wenye uweledi katika nchi mbalimbali.

Katika kiwango cha kitaifa: Shirika linaweza kutoa msaada wa kuwapatia wataalamu wenye uelezi wa usalama barabarani katika nchi zaidi ya 170 na jopo la wataalamu hao wanapatikana katika nyanja za usalama barabarani toka nchi zifuatazo :- Brazil, Cambodia, China, India, Kenya, Mexico, Urusi, Uturuki na Vietnam.

Katika Kiwango cha Kimataifa: Shirika lina jopo la Wataalamu wa kimataifa ambao wanaweza kutoa msaada popote kwenye mambo ya msingi kama sekta za sheria, ukusanyaji wa takwimu na tathmini. Hili jopo la wataalamu wana uweledi wa kuleta ufanisi , misingi ya utekelezaji wa kutoa taarifa, mchanganuo maalum na rasilimali nyingine za kitaaluma

Nyanja zenye kuhusiana: Shirika linaweza kuunganisha vyombo vya habari na wataalamu , rasilimali na vitendea kazi katika maeneo mengi yenye kuhusiana na usalama barabarani, usafiri, mipango miji, watunga na watekelezaji wa sheria, vyama vya wahanga, miundombinu, kanuni na sheria zenye viwango vya utekelezaji.

Kupata wataalamu kwenye eneo lolote kati ya haya, tafadhali wasiliana na: Laura Sminkey tembelea tovuti sminkeyl@who.int au piga simu: +41 22 791 4547

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kushirikiana na Shirika la Afya Duniani

WAJIBU WA SHIRIKA LA AFYA DUNIANI (WHO) USALAMA BARABARANI:

"Suala la Usalama barabarani ni muhimu na lina changamoto kubwa" asema Dkt. Margaret Chan, 2013, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (WHO)

Shirika la Afya Duniani (WHO) ni Shirika la kimataifa lililojikita katika afya ya Jamii. Shirika lina wajibu wa kutoa miongozo ya afya ulimwenguni na kuendeleza ajenda za utafiti na kutumia ushahidi wake katika kuweka miongozo, kanuni za afya na viwango vilivyothibitishwa na sera. Shirika hutoa msaada wa kitaalamu kwa nchi, kufuatilia na kutathmini mipango na mienendo ya afya duniani.

Kwa kuwa ajali za barabarani zinachukua nafasi ya saba kwenye orodha ya visababishi vya vifo; Shirika hilo, imeamua kuwa mtetezi wa usalama barabarani ulimwenguni na limeainisha kuwa tatizo hili ni janga la afya katika jamii mbalimbali na ngazi zote kimataifa na kitaifa. Shirika linasaidia nchi kutekeleza mipango na hatua zilizowekwa ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na usalama barabarani.

Kuboresha viwango vya taarifa za Usalama Barabarani

Ili kufanya maamuzi ya kuandaa sera ya nchi ya Usalama barabarani lazima kuwepo na takwimu sahihi. Licha ya serikali kujua idadi, nani, wapi na kwa nini wamekufa kwa ajali barabarani, pia serikali zinatakiwa kuwa na taarifa kuhusu majeruhi na sababu au viashiria vya hatari- kwa mfano, kujua ni asilimia ngapi ya waendesha pikipiki wanaovaa kofia ngumu na ni asilimia ngapi za ajali zimesababishwa na ulevi. Taarifa hizi zitasaidia serikali kuwa na taarifa sahihi na ushahidi katika juhudi zake za kufuatilia na kutathimini –Hii ina maana kwamba ,ukusanyaji wa takwimu lazima ufuate na kuzingatia vigezo na utaratibu uliokubalika ambao utaunganisha sekta mtambuka mfano polisi na afya ili kuwa na takwimu moja inayofanana nchini.

Mfumo mzuri wa ukusanyaji wa taarifa unasaidia kuleta picha halisi ya ukubwa wa tatizo na kuwa na sera nzuri zinazotokana na ushahidi. Takwimu sahihi zinawezesha kutathmini ufanisi wa sera na mipango iliyowekwa.

Imegundulika kwamba, katika nchi za vipato vya chini na vya kati, takwimu za vifo huonyesha ni za kiwango cha chini sana ukilinganisha na hali halisi. Hivyo, Shirika linashirikiana na nchi ili kuboresha ukusanyaji wa takwimu pamoja na kuendelea kutoa maana na tafsiri kamili ya vifo vinavyotokana na ajali za barabarani na majeruhi.

Kwa taarifa zaidi kuhusu ukusanyaji wa taarifa za usalama barabarani tembelea tovuti "Data Systems: A road safety manual for decision maker and practitioners."

Maana na tafsiri ya vifo vinavyotokana na ajali za barabarani na majeruhi

Katika baadhi ya nchi, taarifa za ajali za barabarani zinajumuisha wale watu ambao hufa kwenye eneo la ajali tu; lakini Shirika linataka wajumuishwe hata idadi ya wale waliokufa siku 30 baada ya ajali kutokea na majeruhi katika taarifa zitakazokusanywa na polisi. Kwa sasa, ni nchi 92 tu zinazotumia tafsiri hii ya Shirika.

Ufuatiliaji na Tathmini

Kadri nchi inavyotoa kipaumbele katika suala la usalama barabarani, kufuata na kuboresha sera , ufuatiliaji na tathmini huwa ni kigezo au kiashiria cha kupanga mipango madhubuti na endelevu. Shirika hukusanya, hufanya upembuzi yakinifu na kutathmini taarifa mara kwa mara kwenye maeneo yafuatayo:

1. Mifumo ya kitaasisi za usalama barabarani
2. Kuangalia hali za barabara kama zinapitika
3. Magari salama kwa matumizi
4. Usalama wa watumia barabara (Waenda kwa miguu, wenye mikokoteni,baiskeli nk)
5. Hudumu za dharura kwa majeruhi baada ya ajali kutokea.

Kazi hii ya ufuatiliaji inafikia kikomo kwa kuandika **ripoti ya Ulimwengu ya hali ya Usalama barabarani** ambapo ripoti yake ya kwanza ilichapishwa mwaka 2009. Ripoti hii, huelezea taarifa za usalama barabarani kwa kina kwa kila nchi angalau kila baada ya miaka miwili -kwa kutumia mbinu/taratibu zile zilizokubalika za kulinganisha katika nchi na mataifa.

Usalama barabarani kuwa ajenda ya kipaumbele

Watunga sera wote duniani hawana budi kutoa kipaumbele kwa kupunguza vifo na majeruhi kwa kuhakikisha kuwa usalama barabarani unadhibitiwa hasa katika nchi zenye kipato cha chini na cha kati ambako vifo vitokanavyo na ajali ni vingi zaidi. Pia, utashi wa kisiasa na ushahidi utasaidia kufanya mipango na maamuzi sahihi yanayohusu usalama barabarani. Kwa mfano, kutoa amri ya kuvaa kofia ngumu kwa madereva na abiria wote, kupunguza mwendo kasi kwenye maeneo ya shule au kupunguza kiwango cha ulevi (BAC) kwa madereva vijana - hizi zote ni jitihada na ushahidi uliothibitika ili kuhakikisha kwamba suala la usalama barabarani linakuwa ni ajenda katika serikali.

Ili kuhakikisha kwamba suala la usalama barabarani linakuwa ajenda kwa serikali, Shirika linakuza na kuratibu mipango na m**iongozo ya utekelezaji wa usalama barabarani; mfano Mkakati wa Muongo mmoja wa usalama barabarani 2011-2020 (UN Decade of Action for Road Safety 2011-2020) ambao unakaribisha wadau wote wa usalama barabarani Ulimwenguni kubadilishana ujuzi, uzoefu na taarifa za kuzuia ajali. WHO pia ni mratibu wa Ushirikiano wa Umoja wa Mataifa wa Usalama barabarani (UNRSC) ambao ni Mratibu wa mashauriano usio rasmi wenye ushirikiano na mashirika ya Umoja wa Mataifa kutekeleza maazimio ya Umoja wa Mataifa na mapendekezo ya ripoti za Shirika la Afya Duniani .**

Shirika la Afya Duniani (WHO) kwenye eneo la kazi: utekelezaji wa usalama barabarani ulimwenguni

Tangu 2009, mipango ya usalama barabarani imekuwa ikitiliwa mkazo na Shirika la Afya Duniani ,kwenye nchi 9 ambazo hufikisha asilimia 60 ya vifo vya barabarani: Nchi hizo ni Brazil, Cambodia, China, India, Kenya, Mexico, Urusi , Uturuki na Vietnam. Shirika, limekuwa likifanya kazi kwa kushirikiana na serikali za nchi hizi kwa kupitia **Bloomberg Philanthropies Programu ya Usalama Barabarani ulimwenguni (BP-GRSP)**, mpango ambao una dhamira ya kupunguza majeruhi na vifo vinavyosababishwa na ajali za barabarani.

Katika kiwango cha kitaifa, Shirika kwa kushirikiana na serikali na wadau wa usalama barabarani kutekeleza mipango inayohusu **viashiria vya hatari vitano** kwa **l**engo la kuhakikisha yafuatayo:-

- **Kuwa na sheria kali za usalama barabarani**: Hatua hii italeta ufanisi na kuleta ushawishi wa kubadili tabia na kuwa na tija katika usimamizi wa sheria. Shirika litasaidia nchi kutathmini sheria au miswada, kuangalia mapungufu na kutoa vipaumbele kwa maeneo ya kurekebisha ili kuleta ufanisi katika mipango ya sasa na ya baadae.
- **Uhamasishaji na Uelimishaji miongoni mwa watumia barabara kuhusu viashiria na tabia hatarishi:** Shirika hushirikiana na serikali kutengeneza matangazo yenye ukweli